Toleo 47

# Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

## DHAMBI ILIPOZIDI

Ulimwengu uko gizani na dhambi zinaendelea kuongezeka. Akili na mioyo ya wanadamu inapofushwa na ari na tamaa za mwili. Ulimwengu unaendelea kwenda mbali zaidi na Neno lake Mungu. Watu wanaojiita Wakristo wanaendelea kukumbatia mawazo ya uhuru wa kidunia. Sio tu kwamba siku hizi ndoa haichukuliwi kuwa pingu ya maisha, bali hata haionekani kwamba ni lazima hiyo ndoa iwe ya uhusiano kati ya mwanaume na mwanamke. Je, tumaini litapatikana wapi kwenye kizazi hiki kiovu?

Miaka mingi iliyopita mhubiri wa injili aliingia kwenye chumba cha hospitali cha mwanaume mmoja aliyekuwa shoga, na ambaye alikuwa karibu kufa kwa ajili ya UKIMWI. Huyu mwanaume ambaye alionekana kwamba anaishi siku zake za mwisho alikuwa amelala hapo kwenye kitanda cha hospitali huku amevalia gauni la kike. Ndipo hapo mchungaji huyo akamwomba kama angemruhusu kuzungumza naye.

Huyo kijana akajibu, "Sitaki kuongea na wewe. Hakuna kitu kingine unataka kuniambia isipokuwa kwamba nitaenda jehanamu nikifa."

Mhubiri naye akamjibu, "La, hasha. Mimi nataka kukwambia kuhusu upendo wake Mungu kwako."

Mchungaji akaanza kumwambia kijana huyo aliyekuwa shoga na ambaye alikuwa akiishi maisha ya dhambi nyingi kuhusu upendo wa ajabu wa Mungu. Akashiriki naye ukweli wa ajabu wa Yohana 3:16-17, "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye."

Jinsi mchungaji aliendelea kunena kuhusu upendo wa Yesu na vile alikuja ili atuokoe kutokana dhambi zetu ndivyo machozi yalianza kumtiririka kijana huyo ambaye alikuwa karibu kufa. Ndipo hapo kijana huyo akafanya ombi kwa Bwana na kumwambia Mungu amsamehe kwa ajili ya dhambi zake zote. Na mara moja kijana huyo akafanyika kuwa kiumbe kipya ndani yake Yesu Kristo. Mambo yote ya kale yakapita na kila kitu kikafanyika kuwa kipya (2 Wakorintho 5:17). Huenda ikawa yeye alikuwa amekataliwa na watu wa familia yake, huenda ikawa yeye alikuwa chanzo cha uchungu mwingi kwa watu waliokuwa wa karibu naye, huenda ikawa alikuwa ameishi maisha ya dhambi na upotovu mkuu, lakini Mungu alimpenda na kumkubali. Aliweza kuoshwa na damu ya Yesu Kristo na kufanyika kuwa mtu safi kabisa.

Mara moja kijana huyo akamwita muuguzi na kuomba apewe vazi la kawaida la hospitali. Hii ilikuwa ni ishara moja ndogo ya toba ya kweli ambayo kijana huyo alikuwa amefanya machoni pake Mungu. Pia akamwomba mhudumu huyo wa injili ahubiri katika mazishi yake. "Marafiki zangu wengi ambao ni mashoga watakuwa kwenye mazishi yangu. Ningetaka uwaambie kile ulichoniambia, kwamba Mungu anawapenda!"

Bwana asifiwe, Mungu asifiwe sana! Kama vile Daudi alivyosema, "Lakini kwako kuna msamaha" (Zaburi 130:4). Hata leo upendo na msamaha wa Yesu umesambazwa kwa watu wote, bila kujali jinsi dhambi zao zilivyo za upotovu mwingi na mbaya kwa kiasi gani. "Kristo Yesu alikuja ulimwenguni awaokoe wenye dhambi" (1 Timotheo 1:15).

Kuna mwanamke ambaye aliletwa kwa Yesu na viongozi wa kidini. Yeye alikuwa ameshikwa akifanya uzinzi na mara moja akafanywa

*(Endelea katika Ukurasa 2)*



"Hata leo upendo na msamaha wa Yesu umesambazwa kwa watu wote, bila kujali jinsi dhambi zao zilivyo za upotovu na mbaya kwa kiwango gani."


Tahariri 3

Mafundisho ya Biblia: Ushoga na Upotovu wa Aina Zingine 4

Ushoga na Upotovu wa Aina Zingine 5-6

Maswali na Majibu 7

Je, Wajua?

Neno Linalofaa kwa Msimu Huu 8

(Inaendelea kutoka Ukurasa 1)

kupatana na hukumu na adhabu yake. Lakini Yesu akamwambia, "Wala mimi sikuhukumu. Enenda zako; wala usitende dhambi tena" (Yohana 8:11). Wakati watu wengine walikuwa wakimhukumu mwanamke huyo, yeye alipata mahali pa kukubalika ndani yake Yesu. Yesu alimpatia tumaini na hakumwacha aendelee kudumu dhambini. Hata ingawa ulimwengu unasema upendo wa Yesu unakubali dhambi, upendo wa kweli na nguvu zake Yesu unamwinua mwanadamu kutoka kwa dhambi zake ili aweze kutotenda dhambi tena.

Kuna mwanamke mwingine ambaye Kristo alikutana naye kando kando mwa kisima cha maji. Mwanamke huyo akasema kwamba yeye hana bwana. Naye Yesu akamwambia alikuwa akisema kweli, "Kwa maana umekuwa na waume watano, naye uliye naye sasa siye mume wako; hapo umesema kweli" (Yohana 4:18). Ndipo Yesu akamwambia kuhusu maji yenye uhai ambayo yangezima kiu cha nafsi yake. Watu wengi wako katika hali moja na mwanamke huyo. Hata ingawa yeye alikuwa akitoka katika uhusiano mmoja na kuingia kwa mwingine mara moja, shauku yake kamwe haikuridhika. Watu wanatafuta raha na tamaa za kimwili huku wakijaribu kupata kusudi la kuishi, kujitambua, na kupata tosheleko. Lakini kwa sababu mambo hayo hayatoshelezi, ndiposa wao wanajiingiza zaidi na zaidi katika dhambi, huku wakitafuta bila kupata amani ya kweli. Bwana Yesu alikuja na kufanya huduma ambayo inamfikia mtu hadi nafsini mwake. Na ni wakati watu tu wanapojitolea kwa Yesu Kristo na kuachana na dhambi zao, ndipo wanapata amani ya kweli na kujihisi kukubalika.

Mtume Paulo alinena na Wakristo wa Korintho na kuwaeleza kuhusu wale ambao hawatarithi ufalme wa Mungu: waasherati, wazinzi, wafiraji, walawiti, walevi, n.k. Na akaendelea kusema, "Na baadhi yenu mlikuwa watu wa namna hii; lakini . . ." (1 Wakorintho 6:11). Ni furaha kubwa kuyasikia maneno kama hayo katika kizazi hiki chetu kilichojaa uovu. Haijalishi kiwango cha dhambi alichotenda mtu, au aina ya maisha ambayo anaishi, kunao wokovu ambao unaweza patikana na watu wote.

"Dhambi ilipozidi, neema ilikuwa nyingi zaidi" (Warumi 5:20). Neema yake Mungu ingaliko na ina nguvu zaidi kushinda tamaa zote na pingu za kimwili. Basi hebu wewe enda uwaambie watu habari hiyo. Hebu enda uwaambie ulimwengu kuhusu upendo wake Mungu. Hebu waambie kuhusu wokovu. Hebu waambie kuhusu tumaini na amani ambayo inapatikana ndani mwake Yesu Kristo! ■

"Wanaume wanakuwa ni kama wanawake,

na wanawake wanakuwa na tabia za kiume, kinyume na maumbile.

Wanawake wanakuwa ni wake, tena pia waume . . .

Maajabu haya jameni! Mambo maovu kabisa!"

KLEMENTI WA ALEXANDRIA

*(Babu wa kanisa wa zama zile, circa 195)*

# MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

**Neno la Mungu**
2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

**Uhusiano wa Upendo**
Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

**Toba**
Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

**Uzao Mpya**
Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6

**Uhuru Kutokana na Dhambi**
1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

**Ujazo wa Roho Mtakatifu**
Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

**Utakatifu**
Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16, Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

**Ufalme wa Mungu**
Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

**Kanisa**
Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13, Kol. 1:18

**Umoja**
Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

**Kanuni za Kanisa**
Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27, Yn. 13:14-17

**Uponyaji wa Kiungu**
Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

**Utakatifu wa Ndoa**
Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3, I Kor. 7:10-11

**Urembo wa Nje**
I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

**Mwisho wa Nyakati**
2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt. 25:31-46

**Kupenda Amani**
Lk. 6:27-29, 18:20

**Ibada**
Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

**Wajibu Mkuu**
Mk. 16:15

Gazeti la *Ukweli wa Injili* ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwahimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tutembelee katika tovuti yetu ya *www.thegospeltruth.org* na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kupitia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@the gospeltruth.org

# Tahariri



*Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti; nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo.* —2 Timotheo 4:3-4

Mtume Paulo alimhimiza Timotheo kuhubiri Neno. Ndiposa ni ombi letu kwamba Mungu atatusaidia kila mmoja wetu ili tuendelee kuwa waaminifu katika kazi ya kuhubiri, kufunza, na kuishi kulingana na Neno la kweli la Mungu. Katika siku hizi zetu, watu wengi hawasikilizi mafundisho ya kweli. Hata wanapokuwa na kiu cha kujua wao hutafuta wahubiri na wachungaji ambao watawafanya kujihisi vizuri kuhusu maamuzi ya maisha yao, hata wakati maamuzi hayo yako kinyume na ukweli.

Somo la robo hii ya mwaka linahusu swala nzito la ushoga, na maswala ya watu kutambua jinsia zao. Hapo mbeleni somo kama hili lingeonekana kuwa lisilofaa katika jalida kama hili la kiinjili. Lakini itikadi hizi na maisha ya aina hii sasa yamesambaa kote ulimwenguni, na katika jamii ambayo tunaishi ndani mwake sasa, na limekuwa sasa ni jambo ambalo watoto na watu wazima wanakumbana nalo karibu kila siku.

*Tutembelee www.thegospeltruth.org ili kujiandikisha na kupata jarida za mbele.*

Katika kizazi za kisasa kinachoitwa Gen Z (chenye umri wa kati ya miaka 11 hadi 26), asilimia 17-18%, yaani mmoja kwa kila watano, wanajitambua kuwa ni mashoga, wa kiume au kike, watu walio na sehemu nyeti za kike na kiume, wanaovutiwa na watu wa jinsia zote mbili kwa mambo ya kingono, na ambao pia wanafanya ngono na jinsia zote mbili; watu ambao hawajitambui kwa jinsia zao za kuzaliwa, waliobadilisha jinsia zao, na wale wasiojitambulisha na jinsia yoyote ile. Basi hili ni swala kubwa mno wakati huu wetu. Na kutokana na athari hizi ambazo zimetuzunguka, idadi inayokua ya vijana watapatwa na mvutano ndani mwao, na pia maswali na majaribu kuhusiana na swala hili.

Sisi kama Wakristo tunastahili kuwa tayari kujadili swala hili, kwa maana ni swala linalojadili katika Biblia. Ikiwa hatutangaza ukweli, basi sauti ya pekee itakayosikika ni ile ya vuguvugu la LGBTZ+, ambalo limekazana sana kufanya upotovu wa mambo ya ngono kuonekana kuwa ni kitu cha kawaida kabisa.

Mimi nilipatwa na huzuni nilipokuwa nikifanya utafiti kuhusu somo hili niliposoma vile watu wanaojiita Wakristo wanabadilisha na kufanya mabadiliko ya maana halisi ya Maandiko, maandiko ambayo ni dhahiri kabisa yanayozungumzia swala hili, katika jitihada za kuyapiga pambaja maisha haya ya dhambi, ili yafanyike kuwa sehemu ya imani ya Kikristo. Lakini hatuna budi kuwa wakweli kwa Neno lake Mungu, kwa maana tutawajibika kwa ajili ya Neno hilo.

Ninakumbuka miaka mingi iliyopita nikisema na mke wangu na kutoa maneno ya kuwadunisha wanaume wawili waliokuwa mashoga na ambao tulikutana nao wakinunua nguo za kike. Lakini Bwana alinikemea na kunijulisha kwamba Yeye alikufa kwa ajili yao. Ninashukuru kwa Yeye kunikumbusha jambo hilo. Yesu anawapenda watu kama hao, na sisi tunastahili kuwa wahudumu wa upendo wake.

Watu wanapoongea dhidi ya tabia za jamii ya LGBTQ+, wao huchukuliwa kuwa ni wenye chuki dhidi ya watu hao, n.k. Lakini kusema ukweli kuhusu dhambi si kumaanisha kwamba sisi ni wenye chuki dhidi ya watu kama hao, si kusema kwamba sisi ni watu wasio na huruma. Hebu basi tuambiane ukweli. Watu wa ukweli wa Mungu wanapenda wenye dhambi WOTE, na wanawaalika waje kwenye ibada zao ili wasikie injili. Watu kama hao wenye tabia hizo za kishoga ni majirani zetu, marafiki zetu, na washirika wa jamaa zetu. Basi ni jambo muhimu kukumbuka kwamba ukweli kuwa mtu anaishi maisha ya dhambi si kusema kwamba yeye hana sifa na hulka nzuri na za kuvutia. Kwa hivyo, hata ingawa sisi tunachukia dhambi na kunena dhidi yake, kwa kweli tunawapenda watu hao.

Ulimwengu umekosa kielelezo cha tabia nzuri, lakini Neno la Mungu na nguvu zake Yesu zinaweza kutengeneza na kufanya upya usafi wa maisha yetu na tabia bora katika jamii kutoka ndani ya mioyo yetu kama wanadamu. Basi mimi nahimiza kila mmoja wetu kuwa macho dhidi ya kupatwa na mielekeo ya kukubali mambo yote kwa misingi kwamba ni jambo bora kuwavumilia na kuwakubali watu wote. Wewe wakubali watu, lakini usikubali dhambi yao na pia usikubaliane na maisha ambayo kwa hakika yako kinyume cha mpango wake Mungu.

Hebu basi Bwana auhurumie ulimwengu wetu, na atusaidie ili tuwe mwanga na nuru ya upendo na tumaini kwa wale ambao wamepotea.

Michael W. Smith

Januari, 2024



# Mwongozo wa Kujifunza Biblia

## Somo: Ushoga na Upotovu wa Aina Zingine

**Masomo ya Maandiko:** *Au hamjui ya kuwa wadhalimu hawataurithi ufalme wa Mungu? Msidanganyike; waasherati hawataurithi ufalme wa Mungu, wala waabudu sanamu, wala wazinzi, wala wafiraji.* —1 Wakorintho 6:9-10

**Muhstasari:** Maandiko yanafundisha kwamba ushoga ni dhambi. Uhusiano wa kimwili au ndoa na mtu ambaye ni wa jinsia yako ni kinyume na maumbile, na pia ni kinyume na mipango yake Mungu kwa ajili ya ndoa. Mungu aliwaumba wake kwa waume; ndiposa jitihada za kisasa za kubadilisha jinsia ya mtu ni kinyume na mipango iliyopangwa na Mungu. Lakini Yesu anawapenda, aliwafia, na anawasambazia wokovu wake jamii ya washiriki wa vitendo vya LGBTQ+.

### I. Kiwango Halisi cha Ukweli

A. 2 Timotheo 3:16 Maandiko yametolewa na Mungu.
B. Yohana 8:32 Ukweli huleta uhuru.
C. Isaya 5:20-21 Ole wao wasemao kwamba uovu ni wema.

### II. Agano la Kale Linalaani Ushoga na Watu Kufanya Ngono na Wanyama

A. Walawi 18:22-24 Usilale na mwanamume mfano wa kulala na mwanamke.
B. Walawi 20:13-16 Ushoga na kufanya ngono na wanyama ni chukizo.

### III. Tabia za Kishoga Ni Kinyume na Mafundisho ya Agano Jipya

A. Warumi 1:24-28 Matendo ya kishoga huongozwa na tamaa, ni maovu, na yako kinyume na maumbile.
B. 1 Wakorintho 6:9-11 Wafiraji na walawiti.
C. 1 Timotheo 1:9-10 Ushoga ni kinyume na utauwa.

### IV. Usherati Ni Dhambi

A. Wakolosai 3:5-6 Kuua tamaa mbaya.
B. Mathayo 15:19-20 Uzinzi na usherati hunajisi.
C. 1 Wakorintho 6:18 Dhambi dhidi ya mwili.
D. Wagalatia 5:19-21 Matendo ya mwili.

### V. Ndoa Ni Kati ya Mwanaume na Mwanamke

A. Mwanzo 2:18, 22-24 Mungu ndiye aliumba ndoa ya mwanaume mmoja na mwanamke mmoja.
B. Mathayo 19:5-6 Mume na mke ni mwili mmoja.
C. Waefeso 5:31 Mume na mke wake wameunganishwa pamoja.

### VI. Kutambua Jinsia

A. Mwanzo 1:27-28 Tuliumbwa ili tuzaane.
B. Mathayo 19:4 Mungu aliwaumba wake kwa waume.
C. Kumbukumbu 22:5 Kuvaa nguo za jinsia nyingine ni chukizo.
D. 1 Wakorintho 6:9 Ufiraji—Tamaa za kimwili na kujiburudisha kwa njia sisizofaa.

### VII. Hukumu ya Kiungu

A. Mwanzo 19:1-14 Sodoma na Gomora.
B. Yuda 1:7 Waasherati wataadhibiwa katika moto wa milele.

### VIII. Msinyeshwe Roho wa Ulimwengu

A. Warumi 12:2 Msiifuatishe namna ya dunia hii.
B. 1 Wakorintho 2:12-13 Msiipokee roho ya dunia.
C. 1 Wakorintho 3:18-19 Hekima ya ulimwengu huu ni upuzi.
D. 1 Yohana 2:15-17 Msiupende ulimwengu

### IX. Mungu Anawapenda Washiriki wa Vitendo vya LGBTQ+

A. Yohana 3:16 Kwa maana Mungu aliupenda ulimwengu.
B. Warumi 5:8 Kristo alikufa kwa ajili yetu tulipokuwa tungali wenye dhambi.

### X. Mapatanisho na Wokovu Ni kwa Ajili ya Watu Wote


A. 1 Yohana 1:9 Mungu atatutakasa dhambi zote.
B. 2 Wakorintho 5:17-18 Ndani yake Kristo mambo yote ni mapya.
C. Ufunuo 22:17 Yeyote atakaye.

### Tamati

*Na baadhi yenu mlikuwa watu wa namna hii; lakini mlioshwa, lakini mlitakaswa, lakini mlihesabiwa haki katika jina la Bwana Yesu Kristo, na katika Roho wa Mungu wetu.* —1 Wakorintho 6:11

# Ushoga na Upotovu wa Aina Zingine

Mungu aliwaita watu wake ili kuishi maisha safi, maisha matakatifu, maisha yanayoambatana na mpango wake wa kiungu, kwa wanawake na wanaume. Ndiposa tunasema kwamba, hata ingawa matendo ya ushoga na ubadilishaji wa jinsia ni jambo linaloendelea kukubalika katika utamaduni wetu, katika siasa na hata katika dini, Neno la Mungu linatambua mambo haya kama yasiyolingana na maisha ya utauwa, kwamba ni matendo ya dhambi.



"Ukweli haubadiliki, haijalishi kiwango cha upotovu na kukubalika kwa mambo mabaya katika jamii."

## Kiwango Halisi cha Ukweli

Ukweli haubadiliki, haijalishi kiwango cha upotovu na kukubalika kwa mambo mabaya katika jamii. Kwa fikira za kilimwengu, hakuna ukweli ambao hauwezi kubadilishwa, na kila kitu huchukuliwa kwamba kinategemea mambo yalivyo wakati huo duniani. Lakini biblia ndio Neno la Mungu lililovuviwa (2 Timotheo 3:16), na ndani mwake kunapatikana ukweli wa pekee ambao utamwongoza mtu kufika Mbinguni. Ukweli wa Neno la Mungu utawafanya watu kuwa huru kabisa, ili wawe na amani kwa Mungu na ndani mwao. Nabii Isaya alitangaza "ole wao" kwa wale "wasemao kwamba uovu ni wema, na kwamba wema ni uovu; watiao giza badala ya nuru, na nuru badala ya giza" (Isaya 5:20). Hii ndiyo hali halisi ulimwenguni huu, na kwa hivyo ni jukumu letu kama watu wa Mungu kusimama wima, sio tu katika upendo, bali pia katika ukweli. Mafundisho ya Neno la Mungu ndiyo ambayo yanastahili kuchukuliwa kuwa kiwango cha ukweli; na athari na misimamo ya kidunia haistahil kupewa nafasi ya kuongoza misimamo yetu kwa swala la maisha ya jamii na matendo ya ushoga wa washirika wa LGBTQ+.

Vuguvugu hilo la kutetea ushoga wa kike na kiume lina nguvu nyingi; kwa hivyo, linavunjilia mbali misingi ya jamii na kuleta changamoto kwenye mpango wa familia ambao uliwekwa na Mungu. Ushoga na ubadilishaji wa jinsia ni mambo ambayo sasa yanafanywa kuwa ya kawaida kupitia kwa vyombo vya habari na uburudishaji wa watu. Na hata ingawa mtu binafsi anaweza kuwa hayakubali maisha hayo, kuna watu wengi ambao hawajali kuhusu mambo hayo na hata wanayakubali kuwa ni sehemu ya kawaida ya jamii. Lakini ushoga, ubadilishaji wa jinsia, na watu kufanya ngono na wanyama, ni mambo ambayo yamelaaniwa katika Neno la Mungu. Na kwa hivyo, hata ingawa silo jambo linalokubalika kwa wengi mtu kusema ukweli wa mambo halisi, sisi tunasema kwamba matendo ya washirika wa LGBTQ+ ni dhambi.

## Agano la Kale Linalaani Ushoga na Watu Kufanya Ngono na Wanyama

Agano la Kale linalaani ushoga. "Usilale na mwanamume mfano wa kulala na mwanamke; ni machukizo. Wala usilale na mnyama ye yote, ili kujitia unajisi kwake; ... ni uchafuko. Msijitie unajisi katika mambo hayo hata mojawapo; kwa maana hizo taifa nitakazozitoa mbele zenu zimekuwa najisi kwa mambo hayo yote" (Walawi 18:22-24). Sheria ilisema kwamba wanaotenda matendo kama hayo wanastahili kuuawa (Walawi 20:13-16).

## Mafundisho ya Agano Jipya

Hata ingawa sisi hatuishi chini ya hukumu za Sheria za Musa, Agano Jipya linafundisha kwa njia ya wazi kabisa kwamba ushoga ni dhambi. Kwa sababu wanadamu walianza kujiabudu wao wenyewe zaidi ya vile walimwabudu Muumbaji kwa njia ya tamaa zao, Mungu aliwaachilia kufanya mambo potovu kabisa. "Wanawake wakabadili matumizi ya asili kwa matumizi yasiyo ya asili; wanaume nao vivyo hivyo waliyaacha matumizi ya mke, ya asili, wakawakiana tamaa, wanaume wakiyatenda yasiyopasa" (Warumi 1:24-28). 1 Wakorintho 6:9-11 imetoa orodha ya watu ambao hawataurithi ufalme wa Mungu. Kati yao kuna "wafiraji na walawiti." Huu ndio ushoga wenyewe. Wale ambao ni "Wafiraji na walawiti" wanajumuishwa kati ya wasiotii sheria, waasi, wasiofuata taratibu, na makafiri (1 Timotheo 1:9-10).

## Usherati ni Dhambi

Uasherati wa aina yote ni dhambi, iwe ni uzinzi au zinaa inayofanywa na jinsia zote mbili. Wakolosai 3:5-6 inawaambia watu "ifisheni viungo vyenu vilivyo katika nchi, uasherati, uchafu, tamaa mbaya." Naye mtume Paulo alitushauri "Ikimbieni zinaa . . . yeye afanyaye zinaa hutenda dhambi juu ya mwili wake mwenyewe" (1 Wakorintho 6:18). Wale wanaofanya uzinzi, zinaa, mambo ya uchafu n.k. hawataurithi ufalme wa Mungu (Wagalatia 5:19-21). Watu kulalana kimwili ni jambo ambalo linakubalika tu kati ya wale wenye uhusiano wa ndoa, kati ya mwanaume na mwanamke.

## Ndoa Ni Kati ya Mwanaume na Mwanamke

Ndoa imekosa kufahamika vizuri kwenye utamaduni wetu, na hata kupewa maana isiyo ya kweli. Lakini

*(Endelea katika Ukurasa 6)*

*(Inaendelea kutoka Ukurasa 5)*

tangu mwanzo Mungu alimuumba mwanaume na mwanamke, Adamu na Hawa, ili wadumu pamoja katika ndoa wakiwa mwili mmoja (Mwanzo 2:18, 21-24). Mungu hakuwaumba wanaume wawili au wanawake wawili ili kwamba uhusiano huo wa karibu uweze kutimia. Ndoa inayolingana na Biblia ilikuwa, na daima itakuwa, kati ya mwanaume na mwanamke. Yesu mwenyewe alitilia mkazo ukweli huu katika Mathayo 19:5-6: "Kwa sababu hiyo, mtu atamwacha babaye na mamaye, ataambatana na mkewe; na hao wawili watakuwa mwili mmoja? Hata wamekuwa si wawili tena, bali mwili mmoja. Basi aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe." Tabia zingine zote zinazohusu kukubalika kwa ndoa kati ya waume wawili au wake wawili ni upotovu wa mpango wake Mungu.

## Kutambua Jinsia

Ushoga sio kitu kipya, ni jambo ambalo limekuwako kwa maelfu ya miaka. Lakini katika ulimwengu wetu wa sasa, kwa vile ambavyo jambo hili limeendelea kukubalika, sasa tumefikia uovu wa hali ya juu zaidi katika miaka michache iliyopita. Sio tu kwamba watu wanachagua jinsia ambayo itawavutia kwa mambo ya kingono, bali pia wao wenyewe wanajichagulia jinsia ya miili yao itakuwa gani, sio kwa misingi ya biolojia, bali kwa hiari yao wenyewe. Watu wanabadilisha kitambulisho chao cha jinsia hivi kwamba wanaume wanaanza kuwa na tabia za wanawake, na wanawake nao wanakuwa na tabia za kiume. Isitoshe, wengine wao wanachagua kuwa na tabia zinazolingana na za wanyama. Inashangaza jinsi ulimwengu wetu ulivyoanguka, hivi kwamba sasa unakubali na kuhimiza mambo kama haya kutendeka!

"Basi bila kuzingatia maisha na dhambi ambayo mtu ametenda, "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote" (1 Yohana 1:9).

Mwanzo 1:27 inafundisha kwamba, "Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba." Basi ni jinsia mbili tu zinatambulika na kupatikana katika Maandiko: wanaume na wanawake. Jinsia ya mtu silo jambo la yeye kujichagulia, bali ni jambo linalotokana na biolojia, pamoja na maumbile yake ya chembechembe za DNA. Kwa hivyo kuvuka mipaka hii kwa njia ya mavazi, kwa njia ya upasuaji, au kwa kunywa dawa za kubadilisha maumbile ya asili, ni kitu ambacho ni kinyume na vipawa vya asili ambavyo Muumbaji wetu alitupatia. Mapungufu ya kuzaliwa ambayo yanaweza kumfanya mtu awe na jinsia ambayo haijakamilika vizuri ni chini ya asilimia 0.05%, na jambo hili halistahili kuchukuliwa kuwa ni la kawaida. Ni jambo la kuhuzunisha kwamba watoto huzaliwa wakiwa na kasoro za maumbile, lakini kwa kweli hili ni jambo ambalo linatokea katika ulimwengu wetu. Lakini upungufu huu wa maumbile ambao wakati mwingine hujitokeza hauwezi kufanywa kuwa ni msingi wa watu kwenda kinyume na mpango wa Mungu, hivi kwamba kitambulisho cha jinsia ya mtu likafanywa kuwa ni jambo la mtu kujichagulia mwenyewe.

Basi tabia hizi za sasa za watu kubadilisha jinsia zao ni dhambi, na ni jambo lililokatazwa na Mungu. Kuvaa mavazi yasiyo ya jinsia yako ni jambo linalolaaniwa katika Kumbukumbu 22:5 "Mwanamke asivae mavazi yampasayo mwanamume, wala mwanamume asivae mavazi ya mwanamke; kwa maana kila afanyaye mambo hayo ni machukizo kwa BWANA, Mungu wako." Hata inagwa andiko hili linawakataza wanawake kuvaa mavazi ya wanaume, hasa mavazi ya kivita, pia inasema kwamba mwanaume hastahili kuvaa mavazi ya wanawake. 1 Wakorintho 6:9 inasema kuhusu "ufiraji." Hii inamaanisha kuvaa mavazi mororo ya bei ghali ni jambo linalodokeza tabia za watu za kujifurahisha kwa mambo mapotovu. Je, si mwanaume ambaye anavaa vazi na kuwa na tabia za kike anaweza kusemekana kuwa ndiye anayesemwa hapa? Tunahitaji kukubali jinsia yetu kwa misingi ya biolojia, bila kufanya jitihada zozote za kuibadilisha, kuirekebisha, au kuwa na tabia za jinsia ile nyingine.

## Hukumu ya Kiungu

Kilio cha Sodoma na Gomora kinafika mbinguni tena. Moto na kibiriti vilimwagwa katika miji hiyo kwa ajili ya hukumu ya Mungu iliyotokana na dhambi zao mbaya zilizolingana na somo tunalolisoma kwa sasa (Mwanzo 19:1-14). Yuda 1:7 inatuonya: "Kama vile Sodoma na Gomora na miji iliyokuwa kando-kando, waliofuata uasherati kwa jinsi moja na hawa, wakaenda kufuata mambo ya mwili yasiyo ya asili, imewekwa kuwa dalili, wakiadhibiwa katika moto wa milele."

## Roho wa Ulimwengu

Kwa sababu tumezingirwa na tabia mbovu zinazohusiana na maswala ya ngono, na kuambatana na falsafa tofauti tofauti, ni muhimu kwamba sisi tusinyweshe roho wa ulimwengu (1 Wakorintho 2:12-13). "Msiifuatishe namna ya dunia hii; bali . . . mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu" (Warumi 12:2).

## Mungu Anawapenda Washiriki wa Vitendo vya LGBTQ+

Hata ingawa hukumu za Mungu ni za hakika dhidi ya uovu na upotovu wa kila aina wa kizazi hiki kuhusu maswala ya ngono, Mungu awapenda watu wote (Yohana 3:16). Mungu anachukia dhambi, lakini Yeye anawapenda wenye dhambi. Yesu alikufa kwa ajili ya wenye dhambi wote, na kila mmoja wetu alikuwa akiishi wakati mmoja kama mwenye dhambi. Basi bila kuzingatia maisha na dhambi ambayo mtu ametenda, "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote" (1 Yohana 1:9). Mungu anaweza kumchukua mwenye dhambi mkuu na kumfanya kuwa mtu safi. Yesu hakuja kuwahukumu watu, bali kuwaokoa kutokana na dhambi zao. "Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya" (2 Wakorintho 5:17).

## Wokovu Ni kwa Ajili ya Watu Wote

Basi tusife moyo, bali tuwe imara katika ukweli wa Neno lake Mungu. Hebu basi tuwaombee wale ambao wamevutwa na kuingia kwenye mitego inayoongozwa na tamaa za mwili zinazoletwa na adui yetu. Bado kungali na nafasi ya kuyaimarisha maisha yetu, kwa sababu kungali kuna nguvu ndani yake Kristo, nguvu zinazobadilisha maisha ya watu. ■

# Maswali na Majibu

## Kama Wakristo tunastahili kuwatendelea vipi washirika wa maisha ya LGBTQ+?

Watu binafsi na familia wanaweza kujipata mahali pabaya wakijaribu kujua jinsi ya kuwatendea watu wanaoishi maisha yanayolingana na yale ya LGBTQ+. Lakini katika kila uamuzi wanaofanya, ni muhimu tudumishe roho na upendo wa Kristo. Yesu alikuwa rafiki ya wenye dhambi. Katika Mathayo 9:10-13 Mafarisayo waliuliza ni kwa nini Yesu alikuwa akila na wenye dhambi na watoza ushuru. Yesu akawajibu, "Wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio hawawezi. Lakini nendeni, mkajifunze maana yake maneno haya, Nataka rehema, wala si sadaka; kwa maana sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi."

Yesu hakuwa akishiriki au kuunga mkono matendo ya dhambi ya watu hawa; bali alikuwa akinyoosha mkono wake wa upendo kwao kwa sababu ya nafsi zao. Basi nasi hatuna budi kuwatendea watu wote kwa upendo na heshima kwa maana wao waliumbwa na Mungu, bila sisi kuzingatia vile wanavyoishi. Ikiwa sisi tutawatenga kabisa watu wale wanaoishi gizani, je, watawezaje kukutana na tumaini la wokovu? Yesu pia alifundisha kwamba tunastahili kuwapenda majirani wetu kama tunavyojipenda sisi wenyewe (Mathayo 22:39). Je, katika ulimwengu wetu wa dhambi jirani yetu ni nani? Ni muhimu basi kuwaonyesha watu hao upendo pasi sisi kushiriki katika dhambi zao. Hata ingawa kuna dharao kubwa iliyoko dhidi ya tabia hizi potovu za kingono, dharao hizo zinastahili kuelekezwa kwa matendo yao, sio kwa washiriki wa matendo hayo.

Ni muhimu kukumbuka kwamba kumpenda mtu si kusema kwamba unakubaliana naye, au kwamba unavumilia matendo yake ya dhambi. Katika hali nyingi, mimi nitaona vigumu kuhudhuria ndoa inayotokana na uzinzi au ushoga. Hata ingawa sisi tunawapenda watu, tutaona vigumu kuwaunga mkono au kushiriki katika sherehe kama hizo.

Katika hali nyingine pengine itakuwa ni jambo muhimu sisi kuwa na miongozo kuhusu swala hili, na pia kuweka mipaka ya mahusiano ya pale nyumbani ili kudumisha utauwa humo nyumbani mwako, kwa lengo la kujilinda au kuwalinda watoto wadogo dhidi ya athari potovu. Lakini yote tunayoyasema au kufanya tunastahili kutenda kwa kulingana na roho wake Kristo. Na zaidi ya yote hebu tuwaombee washiriki hao wa matendo ya LGBTQ+ ili nao wapate wokovu. ■

## Je, nifanye nini kama najipata kwamba navutiwa na watu wa jinsia yangu?

Shetani amefanya juu chini kufanya mahusiano ya jinsia moja kuonekana kuwa kitu cha kawaida. Ikiwa mtu anavutiwa na mtu wa jinsia yake, maombi ndiyo silaha kuu ya kupambana na adui na mwili. Kuna uhuru wa kiungu kutoka kwa dhambi na pia kuna mahali ndani yake Kristo ambako majaribu yanaweza kupoteza nguvu zake. Wakati ambapo maroho ya tamaa yanafanya kazi yake kuna uwezekano wa kupata ukombozi. Wakati huu ambapo dhambi potovu za ngono zinazidi kuongezeka katika jamii, majaribu hayo yataendelea kuongezeka. Ujuzi ambao mtu amepitia maishani mwake, hali ambazo yeye anaishi ndani mwake, na mavutio ambayo ni ya kawaida kutokana na maumbile yake, huenda yakawafanya watu wengine kuwa ni rahisi wao kuanguka katika jambo hili kuliko watu wale wengine. Lakini ni muhimu kukumbuka kwamba kujaribiwa sio dhambi; kujisalimu katika majaribio ndio dhambi. "Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili" (1 Wakorintho 10:13).

Pia ni jambo muhimu mwathiriwa wa tamaa hizo kutotia nguvu mavutio hayo. Usitazame mambo au kushiriki na watu ambao watatilia nguvu au kulijenga jaribu hilo ndani yako. Yatoroke mambo yote ambayo yataleta shauku zaidi ya kufanya ndoa ya dhambi. Basi katika vita hivyo vyako wewe endelea kupigana. Muombe Mungu kila siku ili akusaidie kudumisha moyo na mawazo yote kwa mambo mazuri na safi. Hebu jihusishe na kikundi cha Wakristo ambao watakuunga mkono katika jitihada zako na uendelee kukua katika safari yako na Mungu.

Ikiwa hujaoa au kuolewa, usifanye juhudi za kumwoa mtu wa jinsia nyingine kwa lengo la kushinda mavutio hayo. Jambo hilo litakufuata hata katika ndoa hiyo yako na ni jambo linaloweza kukuletea madhara makubwa ndoani. Hebu pata ushindi kwanza, ndipo umtafute Mungu akupatie mwenza wa jinsia nyingine kwa kulingana na mapenzi yake.

Basi sisi tunakuhimiza kwamba kuna nguvu za kushinda dhambi na majaribu; na Mungu ana mahali ndani mwake ambapo wewe waweza kupata ushindi na amani. ■

JE, WAJUA?

"Asilimia 7% ya Wamarekani ni mashoga wa kike au kiume, na pia watu wanaovutiwa na jinsia zote mbili, hii ni kulingana na utafiti wa Pew Research Center uliofanywa kwa idadi ya watu wazima 12,147, na ambao ulifanywa katika msimu wa joto (summer) mwakani 2022. Nayo asilimia 17% ya vijana wazima wasiofikia umri wa miaka 30 wanajitambua kuwa ni mashoga wa kiume na kike, na pia watu wanaovutiwa na jinsia zote mbili; ikilinganishwa na asilimia 8% ya watu wenye umri wa kati ya miaka 30 hadi 49; na asilimia 5% kwa watu wenye umri wa kati ya miaka 50 hadi 64; na asilimia 2% ya watu walio na umri wa miaka 65 au zaidi" [Brown, Anna. Juni 23, 2023. www.pewresearch.org.]


Kati ya nchi 30 zilizofanyiwa uchunguzi, kwa kiwango cha wastani asilimia 3% ya watu walijitambua kuwa ni mashoga wa kike au kiume, asilimia 4% kuwa ni wenye sehemu nyeti za kike na kiume, na asilia 1% kuwa ni watu wa kufanya ngono na jinsia zote, au watu wenye jinsia zote, na asilia 1% kuwa ni watu ambao hawana jinsia yoyote ile." [www.ipos.com (2023)].

Neno Linalofaa kwa Msimu Huu

# MCHUKULIANE MIZIGO

*Mchukuliane mizigo na kuitimiza hivyo sheria ya Kristo.* —Wagalatia 6:2

Kutokana na dhambi sisi tunaishi katika ulimwengu uliovunjika. Watu wanashindana na tabia haribifu, uraibu, na nguvu zinazoletwa na tamaa. Watu wanaishi na upweke na wanatafuta kitambulisho chao cha kibinafsi, mahali pa kupata ushirika, na hata amani. Mahusiano ya kifamilia yanakatika, na ndoa zinavunjika. Watoto nao wanakumbana na athari sisizofaa, na misukumo mikubwa kuliko hapo awali. Nazo shida zinazohusiana na maswala ya afya ya kiakili na kihisia zinazidi kuongezeka. Jinsi ulimwengu unavyoenenda ni jambo linaloharibu maisha ya watu.



Hata ingawa giza linaonekana kujaa, kuna tumaini linalong'aa ndani ya Yesu Kristo. Mbele yetu kuna Mbingu ambako tunaenda, mahali ambapo hakutakuwa na hali hii ya kuvunjika. Katika ulimwengu huu tunakutana na majaribu, lakini kupitia kwa Yesu Kristo tuna mwangaza, tumaini na amani. Basi tuna ujumbe wa ajabu wa kushiriki na watu ambao wanapitia mashindano hayo. Mambo ya ulimwengu huu hayaleti suluhisho la shida ambazo watu wako nazo; badala yake mambo hayo yanayafanya shida hizo kuwa mbaya zaidi. Hebu basi tuseme kwa uwazi kabisa kuhusu tumaini la ajabu la Injili.

Maandiko yanatufundisha kwamba "Tuchukuliane mizigo." Hii inamaanisha kuchukua, kubeba, na kuvumilia kwa subira mizigo ya watu wale wengine. Watu waliovunjika wanahitaji upendo, utunzi, na kukutana na watu wanaowaelewa. Hatuwezi kuwaboresha watu, lakini tunaweza kuwa nao katika shida ambazo wamejipata ndani mwake. Tunaweza kuwasikiliza, kuwaombea, na kushiriki nao tumaini. Na zaidi ya yote tunaweza kuwaelekeza kwa Mwokozi ambaye ana uwezo wa kufanya kile ambacho mwanadamu hawezi kufanya.

Kuwabebea watu wale wengine mizigo si jambo rahisi, lakini huo ndio mwito wetu na jukumu letu. Watu wenye maumivu wanaweza kumletea mtu maumivu; wanaweza kusema maneno makali kwa watu wale ambao wanawapenda. Unapobeba mizigo ya watu wale wengine hebu kumbuka kwamba wao wanaweza kukuletea maumivu. Unapojitoa kwa ajili ya watu wale wengine, wakati mwingine wao watakuletea uchungu kupitia kwa maneno na matendo yao. Hebu basi ona zaidi ya kile wanachosema au kufanya, na kuona jinsi wao walivyovunjika. Watu hao wataenda wapi ikiwa sisi tutawaachilia?

Kama vile ambavyo Mungu amekuwa mwenye subira na mwaminifu kwetu, hebu tutimize sheria ya Kristo na kupeleka subira hiyo na upendo wake kwa watu wale wengine ambao wanapambana ili kupata njia iliyo mwafaka. Hebu tuwaonyeshe Kristo kupitia kwa upendo wetu na vile ambavyo tunawajali. Hebu Bwana Yesu abariki kila mmoja wetu tunapobeba mizigo ya watu wale wengine. ■

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

Utakatifu kwa Bwana